## HALMASHAURI YA MJI KONDOA

**MUHTASARI WA KIKAO CHA BARAZA LA WAHESHIMIWA MADIWANI KILICHOFANYIKA TAREHE 02/11/2022 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI YA MJI KONDOA.**

**Waliohudhuria**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Besela I. Maunga | -D/V/Maalum | - | M/kiti |
| 2. | Mhe. Juma I. Ng'ungu | -D/Kolo | - | Mjumbe |
| 3. | Mhe. Zainabu H. Hemed | -D/Chemchem | - | " |
| 4. | Mhe. Abushehe I. Mbuva | -D/Kingale | - | " |
| 5. | Mhe. Issa I. Kambi | -D/Kilimani | - | " |
| 6. | Mhe. Jafari M. Ganga | -D/Suruke | - | " |
| 7. | Mhe. Rachel M. Sombida | -D/V/Maalum | - | " |
| 8. | Mhe. Kulwa S. Pazi | -D/Serya | - | " |
| 10. | Mhe. Fatuma I. Issa | -D/V/Maalum | - | " |
| 11. | Mhe. Hajat Ramla H. Abedi | -D/Bolisa | - | " |
| 12. | Ndg. Paul M. Sweya | -Mkurugenzi | - | Katibu |

**WAKUU WA IDARA NA VITENGO**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ndg. Salumu Yusuph | -Kny Mkuu Kitengo cha Fedha na Uhasibu |
| 2. | Ndg. Shabani N. Sued | -Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sheria |
| 3. | Ndg. Esther Komba | -Kny Mkuu wa Idara ya Mipango na Uratibu |
| 4. | Ndg. Annette T. Nara | -Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari |
| 5. | Ndg. Hassan Kiseto | -Mkuu wa Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi |
| 6. | Eng. Jeremia Longido | -Kaimu Mkuu wa Idara ya Miundombinu, Maendeleo ya Vijijini na Mjini. |
| 7. | Ndg. Latipha Koshuma | -Kny. Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii |
| 8. | Ndg. Hassan Mtamba | -Mkuu wa Idara ya Elimu ya Awali na Msingi |
| 9. | Ndg Lucy J. Timba | -Mkuu wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu |
| 10. | Ndg.Sekela Mwasubila | -Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini |



CamScanner

11. Ndg. Alfred Chakalike -Kny. Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi wa Taka na Usafi wa Mazingira.

12. Ndg. Manase Shekalaghe - Kaimu Mkuu Wa Kitengo Cha Ukaguzi wa Ndani

13. Ndg. Ramadhan J. Hamis -Kny Mkuu wa Kitengo cha Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira

14. Ndg. Habiba H. Mafita -Mdhibiti Mkuu wa Ubora wa Shule Halmashauri ya Mji Kondoa

15. Dkt. Sisti A. Mosha - Kaimu Mkuu wa Idara ya Huduma ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe

16. Ndg. Godfrey S. Lugano - Katibu Msaidizi wa Tume ya Walimu

**MAAFISA TARAFA**

1. Ndg. Ally R . Mbena - Afisa Tarafa ya Kondoa Mjini
2. Ndg. Fred J. Bangule - Afisa Tarafa ya Kolo

**WAKUU WA TAASISI**

1. Ndg. Wera R. Kweka - Mhandisi TARURA
2. Eng. Bakari J - Mhandisi TARURA

**VYAMA VYA SIASA**

1. Ndg. Hija Bakari Suru - Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi
2. Ndg. Ibrahimu S. Mpwapwa - Katibu wa Chama Cha Mapinduzi

**WAGENI WAALIKWA**

1. Ndg. Leila A. Mhawila
2. Ndg. Mathew Mlele
3. Ndg. Irene M. Venance
4. Ndg. Isack Mgogeja Buyamba
5. Ndg. Emiliana Charles
6. Ndg. Hafidhi Mkanga
7. Ndg. Likadya I. Mwampashe

**HABARI**

1. Ndg. Hussein M. Mwalimu
2. Ndg. Brighton Kimaro
3. Ndg. Nizari Mafita
4. Ndg. Iddi Ibrahimu

**Sekretarieti**

1. Ndg. Rosemary M. Mnguli
2. Ndg. Tatu N. Jabily

**MUHTA NA 08/2022/2023 KUFUNGUA KIKAO**

Kabla ya kufungua kikao mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe wote kwenye kikao aliwashukuru kwa mahudhurio yao mazuri. Alifungua kikao saa 8:30 mchana baada ya kujiridhisha kutimia kwa akidi ya wajumbe.

**Utambulisho.**

Mwenyekiti alitoa fursa kwa watumishi wageni ambao ni ajira mpya kujitambulisha kwenye kikao cha Baraza la Madiwani, watumishi wote walijitambulisha kwa idara ambapo ni watumishi kutoka Idara ya Huduma ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe, Kitengo cha Manunuzi, Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani pamoja na Idara ya Utawala, Usimamizi wa Ralimimali Watu. Wajumbe wote kwa pamoja waliwapokea watumishi hao na kuwaahidi kuwapa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yao.

**MUHTA NA 09/2022/2023 KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKAO**

Agenda zifuatazo zilithibitishwa na kuridhiwa na wajumbe.

1. Kufungua kikao.
2. Kuthibitisha agenda za kikao.
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha tarehe 8/09/2022.
4. Maswali ya papo kwa papo kwa Mhe. Mwenyekiti na Mkurugenzi wa Mji



CamScanner

5. Kupokea taarifa za utekelezaji wa shughuli za Idara kutoka Kamati za kudumu za Halmashauri na Kamati zisizo za kudumu.

    i. Kamati ya Mipango Miji na Mazingira.
    ii. Kamati ya Uchumi, Afya na Elimu.
    iii. Kamati ya Kudhibiti Maambukizi ya UKIMWI.
    iv. Kamati ya Fedha na Utawala.

6. Taarifa mbalimbali kutoka kwa Mwenyekiti pamoja na Mkurugenzi
7. Kufunga kikao.

**MUHT. NA 10/2022/2023 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 08/09/2022**

Baada ya kusomwa na kutokuwa na masahihisho yoyote muhtasari wa kikao cha tarehe 08/09/2022 ulithibitishwa na kusainiwa na kuwa nyaraka halali ya Halmashauri ya Mji Kondoa.

**MUHTA NA 11/2022/2023 MASWALI YA PAPO KWA PAPO KWA MWENYEKITI NA MKURUGENZI**

Hapakuwa na maswali ya papo kwa papo yaliyowasilishwa kwa Mhe. Mwenyekiti na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Kondoa.

**MUHT NA 12/2022/2023 KUPOKEA TAARIFA KUTOKA KAMATI ZA KUDUMU NA ZISIZO ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI.**

Wenyeviti wa Kamati za kudumu na zisizo za kudumu waliwasilisha taarifa za utekelezaji wa shughuli zilizotekelezwa na Idara zilizo chini ya Kamati zao kwa kipindi cha robo ya kwanza Julai - Septemba, 2022 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 katika kikao cha Baraza la Waheshiwa Madiwani. Kamati zilizowasilisha taarifa ni kama ifuatavyo:-

**I. Kamati ya Mipango Miji na Mazingira**

Mwenyekiti wa Kamati ya Mipango Miji na Mazingira aliwasilisha taarifa ya Kamati mbele ya wajumbe wa kikao ambapo alieleza kuwa Kamati inajumuisha Idara moja na vitengo viwili ambazo ni Idara ya Miundombinu, Maendeleo ya Vijijini na Mjini, Kitengo cha Usimamizi wa



CS CamScanner

Taka na Usafi wa Mazingira na Kitengo cha Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira. Alifafanua kuwa Kamati iliketi kikao chake tarehe 19/10/2022 na kujadili taarifa za utekelezaji wa shughuli za Idara zilizotekelezwa kwa kipindi cha robo ya kwanza Julai - Septemba, 2022.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuijadili kisha walihoji kuhusu stendi ya Bicha kufunguliwa na kuanza kufanya kazi. Ufafanuzi ulitolewa kuwa kazi ya kutengeneza stendi inaendelea kwa kuwa fedha tayari zimekwisha idhinishwa hivyo stendi ya Bicha itafunguliwa mapema baada ya kazi kukamilika.Taarifa ya Kamati ya Mipango Miji na Mazingira ilipokelewa na kuridhiwa na wajumbe.

**II. Kamati ya Uchumi, Elimu na Afya**

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Elimu na Afya aliwasilisha taarifa ya Kamati yake mbele ya wajumbe wa kikao ambapo ilielezwa kuwa Kamati ina jumla ya Idara sita ambazo ni Idara ya Huduma ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe, Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Idara ya Maendeleo ya Jamii, Idara Elimu ya wali na Msingi, Idara ya Elimu Sekondari pamoja na taarifa ya iCHF, Taarifa ya TASAF, Tume ya Utumishi wa Walimu na Uthibiti Ubora wa Shule. Alifafanua kuwa Kamati iliketi kikao chake tarehe 17/10/2022 na kujadili taarifa za utekelezaji wa shughuli za Idara zilizotekelezwa kwa kipindi cha robo ya kwanza Julai - Septemba, 2022 Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuijadili na ilihojiwa kuhusu mikakati iliyowekwa ya kupata pembejeo za kilimo ikiwa ni pamoja na mbolea ya ruzuku. Ufafanuzi ulitolewa kuwa usajili wa wakulima katika daftari maalum la wakulima umekamilika na wakulima 4700 wamesajiliwa na kuwekwa kwenye mfumo na kila mkulima atapata namba ambayo ataitumia katika kupata pembejeo ambapo mbolea itatolewa kwa wakulima kupitia namba za usajili zilizopo kwenye mfumo. Ilielezwa kuwa mfuko mmoja wa mbolea utauzwa kwa shilingi 70,000/= na mbegu za Alizeti itauzwa kwa shilingi 5000/= kwa kilo moja.

Aidha, wajumbe walihoji kuhusu mikataba iliyowekwa ya uanzishaji wa kilimo cha umwagiliaji. Ilifafanuliwa kuwa Halmashauri ya Mji Kondoa imekwisha ainisha maeneo kwa ajili ya uwekezaji wa kilimo cha umwagiliaji ambapo Serikali inatekeleza mpango huo kwa awamu na fedha zilikwisha kutengwa kwa ajili ya kuendesha mradi wa kilimo cha umwagiliaji. Hivyo, fedha zitakapopokelewa mradi utaanza kutekelezwa.



CamScanner

Pia Halmashauri imepata mfadhili kutoka Uturuki wa mradi wa DWFP aliyeonesha nia ya kufanya uwekezaji kwenye miradi ya umwagiliaji. Taarifa za msingi amekwishapewa hivyo utekelezaji utafuata baada ya kufanyika kwa upembuzi yakinifu.

Vile vile, ilihojiwa ushiriki wa Waheshimiwa Madiwani katika uibuaji wa kaya masikini katika Maeneo yao. Ufafanuzi ulitolewa kuwa wakati wa zoezi la uibuaji wa kaya masikini Serikali hutoa mwongozo hivyo zoezi hilo wakati wa utekelezaji huwa na utaratibu maalum.

Ilielezwa kuwa Mtaa wa Bicha ulianzisha harambee kwa ajili ya kuchangia ujenzi wa choo cha shule ya msingi Bicha hivyo wajumbe walihitaji kupata tamko kutoka Halmashauri la kuridhia kabla ya kuanza upya kwa uchangishaji wa michango ya kukamilisha ujenzi wa matundu ya vyoo. Ufafanuzi ulitolewa kuwa michango ambayo ilikwisha kukusanywa kutoka kwa wananchi itumike kukamilisha ujenzi ili wanafunzi waendelee kupata huduma wakati taratibu za ujenzi wa matundu mengine ya vyoo zikiendelea kufanyika. Aidha, kuhusu harambee ya uchangiaji, Halmashauri haitoi kibali cha harambee isipokuwa Mtaa unatakiwa kuendelea kukusanya michango kutoka kwa wananchi kwa kuendelea kuwahamasisha pamoja na kuhamasisha wadau wengine kutoka nje ya Mtaa wa Bicha kuchangia.

Aidha, wajumbe walishauri Menejimenti kukamilisha mapema ukaguzi wa matumizi sahihi ya fedha unaofanyika katika Mtaa wa Tungufu pamoja na Mtaa wa Bicha ili kuruhusu kazi za ujenzi wa matundu ya vyoo uweze kuendelea. Pia walishauri wananchi kusomewa mapato na matumizi ya fedha zilizochangwa awali kabla ya kuendelea na zoezi la uchangishaji.

Ilihojiwa kuhusu sababu iliyosababisha magonjwa katika mfumo wa upumuaji kuwa juu. Ufafanuzi ulitolewa kuwa hii inatokana na hali ya hewa iliyopo kwa sasa ya baridi ambayo inapelekea hali ya magonjwa ya mfumo wa upumuaji kuwa juu. Taarifa ya Kamati ya Uchumi, Elimu na Afya ilipokelewa na kuridhiwa na wajumbe.

### III. Kamati ya kudhibiti maambukizi ya VVU na UKIMWI

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudhibiti Maambukizi ya UKIMWI na VVU aliwasilisha taarifa ya utakelezaji wa shughuli za Kamati mbele ya wajumbe wa kikao, ambapo alieleza kuwa Kamati hiyo inajumuisha Idara mbili ambazo ni Idara ya Huduma ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe na Idara ya Maendeleo ya Jamii. Alieleza kuwa Kamati iliketi kikao chake tarehe 18/10/2022 na



CamScanner

kujadili taarifa za utekelezaji wa shughuli za kudhibiti Maambukizi ya UKIMWI na VVU zilizotekelezwa na Idara hizo kwa kipindi cha robo ya kwanza Julai – Septemba, 2022/2023.

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa ya Kamati ya Kudhibiti Maambukizi ya UKIMWI na VVU wajumbe waliipokea na kuiridhia.

**IV. Kamati ya Fedha na Utawala**

Kwa niaba ya Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Utawala Mhe. Diwani ambaye ni mjumbe wa Kamati aliwasilisha taarifa ya Kamati mbele ya wajumbe wa kikao cha Baraza ambapo ilielezwa kuwa Kamati inajumuisha Idara na vitengo sita ambazo ni Idara ya Fedha na Uhasibu, Idara ya Mipango na Uratibu, Idara ya Utawala na Usimamzi wa Rasilimali watu, vitengo vya Manunuzi, Kitengo cha Huduma na Sheria, Kitengo cha Mawasiliano Serikalini na Kitengo cha TEHAMA na Takwimu. Alieleza kuwa Kamati iliketi vikao vyake tarehe 26/09/2022, 28/09/2022 na 24/10/2022 kujadili na kupitisha masuala mbalimbali pamoja na taarifa za utekelezaji wa shughuli za Idara zilizotekelezwa kwa kipindi cha robo ya kwanza Julai - Septemba, 2022. Hivyo, alichanganua taarifa ya mapato na matumizi pamoja na fedha za miradi ya maendeleo zilizopokelewa kama ifuatavyo:-

**a). Mapato na matumizi**

Ilielezwa kuwa Halmashauri ya Mji kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ilikisia kukusanya jumla ya Shilingi 19,912,978,000.00 kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali vya mapato. Pia ilifafanuliwa kuwa Halmashauri ilivuka mwaka na bakaa ya kiasi cha Shilingi 785,078,798.00 kwa mwaka wa fedha 2021/2022 hivyo kupelekea bajeti ya utekelezaji kuwa kiasi cha shilingi 20,698,056,798.00

Aidha, katika kipindi cha mwezi Septemba, 2022 Halmashauri ilikusanya kiasi cha Shilingi 1,257,320,527.00 ambayo ni sawa na asilimia 16 ya makusanyo ya mapato ya mwezi na kufanya jumla ya makusanyo yote ya kuanzia mwezi Julai, 2022 hadi mwezi Septemba, 2022 kuwa kiasi cha shilingi 3,113,108,156.65 ya mapato yote kwa mwaka 2022/2023. Mapato hayo yaliainishwa kama ifuatavyo;-

i. Mapato ya ndani halisi - 205,504,439.47



CamScanner

ii. Mapato ya Kisekta - 139,736,869.75

iii. Ruzuku ya Serikali Kuu (OC) - 184,901,000.00

iv. Ruzuku ya Serikali Kuu Mishahara - 2,499,556,500.00

v. Miradi ya Maendeleo - 586,624,228,43

Vilevile ilielezwa kuwa Halmashauri ilikisia kutumia jumla ya kiasi cha Shilingi 19,912,978,000.00 kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali vya mapato ikijumuishwa na bakaa ya mwaka wa fedha 2021/2022 ya kiasi cha shilingi 785,078,798.00 na kufanya jumla ya makisio ya matumizi ya fedha zote kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kuwa kiasi cha shilingi 20,698,056,798.00.

Aidha, ilifafanuliwa kuwa katika kipindi cha mwezi Septemba, 2022 Halmashauri ilitumia kiasi cha Shilingi 1,257,320,527.00 na kufikisha jumla ya matumizi yote kuwa kiasi cha shilingi 3,113,108,156.65 sawa na asilimia 16 ya makisio ya matumizi ya fedha zote kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Matumizi hayo yaliainishwa kama ifuatavyo;-

i. Vyanzo vya mapato ya ndani halisi - 132,480,221.00

ii. Mapato ya kisekta - 60,956,000.00

iii. Ruzuku ya Matumizi Mengineyo (OC) - 57,867,280.00

iv. Ruzuku ya Mishahara - 2,512,517,990.00

v. Miradi ya Maendeleo - 349,283,665.65

**b). Mapokezi ya fedha na utekelezaji wa miradi**

Ilielezwa kuwa katika Mpango na Bajeti kwa mwaka 2021/2022, Halmashauri iliidhinishiwa Shilingi 6,252,153,000.35 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kwa mchanganuo ufuatao-;

| Na | Chanzo cha Fedha | Kiasi cha Fedha |
|---|---|---|
| 1 | ELIMU BILA MALIPO | 758,930,000.00 |
| 2 | MITIHANI | 400,816,000.00 |



CamScanner

| | | |
|---|---|---|
| 3 | EGPAF | 57,810,000.00 |
| 4 | GLOBAL FUND | 14,169,000.00 |
| 5 | UNICEF | 10,000,000.00 |
| 6 | LISHE | 56,566,000.00 |
| 7 | CHANJO | 45,471,000.00 |
| 8 | TASAF | 1,052,819,000.00 |
| 10 | BUSKET FUND | 107,918,000.00 |
| 11 | BOOST | 1,290,000,000.00 |
| 12 | SEQUIP | 573,000,000.00 |
| 13 | SERIKALI KUU | 1,834,250,000.00 |
| 14 | MFUKO WA JIMBO | 50,386,000.00 |
| **JUMLA** | | **6,252,135,000.00** |

Halmashauri imekuwa ikitenga asilimia 40 ya mapato yake ya ndani (Mapato Halisi) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imetenga jumla ya **Shilingi 348,920,000.00.**

Aidha, ilielezwa kuwa hadi kufikia 30 Septemba 2022, Halmashauri imepokea kiasi cha Shilingi 910,329,558.46 kutoka katika vyanzo vya mapato mbalimbali ambapo kiasi cha Shilingi 485,628,262.46 ni kutoka Serikali Kuu, Shilingi 351,556,296.00 toka kwa wahisani na Shilingi 73,145,000.00 kutoka mapato ya ndani ya Halmashauri ya Halmashauri. Aidha kiasi cha Shilingi 430,000,000.00 kimepokelewa nje ya Bajeti.

**Matumizi ya fedha za mradi**

Ilifafanuliwa kuwa hadi kufikia mwezi Septemba, 2022 Halmashauri ya Mji Kondoa imetumia kiasi cha Shilingi 422,849,558.46 katika Utekelezaji wa shughuli za Miradi ya Maendeleo. Ambapo kiasi Shilingi 15,665,000.00 toka Mapato ya ndani, Shilingi 305,628,262.46 toka Serikali Kuu na Shilingi 101,556,296.00 toka kwa Wahisani. Mchanganuo wa Matumizi ya fedha hizo ni kama ifuatavyo;

a) Fedha za Mapato ya ndani Shilingi 15,665,000.00 Shillingi 11,000,000.00 zimepelekwa kwenye vikundi vya wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu, na Shilingi 4,665,000.00 zimetumika kwenye kutengeneza banda la ng'ombe na mbuzi eneo la Halmashuri lililopo viwanja vya nanenane Nzuguni Dodoma.



CamScanner

b) Fedha toka Serikali Kuu Shilingi 305,628,262.46 zimeshapelekwa maeneo husika Shilingi 121,003,000.00 kwa ajili ya Shughuli za Mitihani na Shilingi 184,625,262.46 uboreshaji wa mazingira ya kufundisha na kujifunzia kwa shule za Msingi na Sekondari.

c) Fedha kutoka kwa wahisani Shilingi 101,556,296.00 zimepelekwa maeneo husika Shilingi 87,161,046.00 zimetumika kuwezesha kaya masikini, Shilingi 2,450,000.00 zimetumika kutekeleza shughuli za mfuko wa kudhibiti maambukizi ya UKIMWI na Shilingi 11,945,250.00 zimetumika kuhamasisha kampeni ya Chanjo ya Polio.

Wajumbe walipokea taarifa hiyo na kuijadili na ilihojiwa kuhusu mikakati iliyowekwa ya kuhakikisha kuwa karo (slabu) la machinjio katika Kata ya Kingale inawekewa uzio. Ufafanuzi ulitolewa kuwa ujenzi wa uzio katika machinjio hiyo utafanyika kupita mapato ya ndani.

Aidha, ilihojiwa kuhusu urejeshaji wa vifaa vya ujenzi wa miradi ya UVIKO -19 vilivyochukuliwa kutoka katika maeneo mengine na kupelekwa katika Shule Shikizi ya Serengeni. Ilifafanuliwa kuwa utekelezaji utafanyika na vifaa hivyo vitarejeshwa katika maeneo husika kulingana na idadi iliyochukuliwa.

Wajumbe walihoji tarehe rasmi ya kufungua stendi ya Bicha ili kuanza kutumika. Ilifafanuliwa kuwa ujenzi wa stendi unaendelea na baada ya kukamilika itafunguliwa pamoja na ujenzi wa choo kinachoendelea kujengwa katika eneo la stendi ya zamani. Taarifa ya Kamati ya Fedha na Utawala ilipokelewa na kuridhiwa na wajumbe.

**MUHT NA 13/2022/2023 TAARIFA MBALIMBALI KUTOKA KWA MKURUGENZI NA MHE. MWENYEKITI.**

Ilielezwa kuwa Serikali Kuu imeanza kuleta fedha za miradi katika Halmashauri ya Mji Kondoa na kiasi cha shilingi 400,000,000.00 kimepokelewa kwa ajili ya ujenzi wa vyumba tisa (9) vya madarasa. Hivyo, alisisitiza Waheshimiwa Madiwani kushiriki katika ujenzi pamoja na kusaidia kuhamasisha wananchi kuchangia nguvu kazi katika utekelezaji wa miradi hiyo.

**NASAHA KUTOKA KWA KATIBU WA CHAMA CHA MAPINDUZI**

Aliwakaribisha watumishi wapya na aliahidi kuwa Chama kitatoa ushirikiano wa kutosha kwa watumishi hao katika utekelezaji wa majukumu yao. Pia alitoa pongezi kwa Vitengo na Taasisi kwa kutekeleza shughuli zao kupitia ilani ya Chama Cha Mapinduzi.



CS CamScanner

Aidha, alisisitiza kuongeza juhudi katika usimamizi na ukusanyaji wa mapato ili miradi inayotekelezwa kupitia fedha za mapato ya ndani ziweze kutekelezeka na kukamilishwa kwa wakati.

**NASAHA KUTOKA KWA MWENYEKITI WA CHAMA CHA MAPINDUZI**

Alitoa pongezi kwa Menejimenti pamoja na Waheshimwa Madiwani kwa namna wanavyotekeleza majukumu ya Halmashauri kwa ushirikiano mkubwa.

Aliomba Waheshimiwa Madiwani pamoja na Menejimenti kumpa ushirikiano wa kutosha katika utekelezaji wa majukumu yake. Alisisitiza usimamizi wa miradi ili kuunga mkono juhudi za Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kwa kusimamia thamani ya fedha katika miradi ya maendeleo iliyoletewa fedha.

Aidha, alitoa pongezi kwa Mhe. Mama Samia Suluhu Hassani Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi zake za kuendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya maendeleo na kutatua kero za wananchi.

**MUHT NA 14 /2022/2023 KUFUNGA KIKAO.**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe wote na aliwatakia safari njema warudipo majumbani mwao alifunga kikao saa 10 : 40 Jioni.

**U m e t h i b i t i s h w a**

| | |
|---|---|
| ................................... | ............................ |
| **Jina**..ANNETTE T' NARA.......... | **Jina**..MOHAMEDI KIBERENGE.......... |
| **Katibu** | **Mwenyekiti** |

..09/02/2023..........

**Tarehe.**



CamScanner